


Prof. Kyallo Wamitila Releases two works a novel and an anthology of poetry.



## Kaza Macho

*Kaza Macho* ni mkusanyiko wa mashairi yanayoonyesha upeo wa juu wa kipawa cha utunzi alichonacho mtunzi wa mashairi yaliyomo. Mashairi haya yametumia lugha ya kitamathali itakayomwachia msomaji taathira ya kudumu kwa namna yanavyozigusa hisia mbalimbali za msomaji. Mashairi katika diwani hii yanaangazia mawanda yote ya maisha ya watu kwa jumla, hasa katika bara la Afrika, yakipiga darubini ndoto na matamania yao, kadhia za maisha yao kijamii, kisiasa, kiuchumi na kihistoria. Hii ni kazi ambayo hataiweka chini yeyote aanzapo kuisoma hadi atakapolisoma shairi la mwisho.

K. W. Wamitila ni mwandishi mwenye tajriba pevu katika uandishi. Yeye ni mtunzi wa vitabu vya kufundisha shuleni, hadithi za watoto, riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Riwaya zake za *Nguvu ya Sala*, *Musabao!*, *Msimu wa Vipepeo* na *Unaitwa Nani?* zimeshinda Tuzo ya Fasilhi ya Jomo Kenyatta katika miaka 2001, 2005, 2007 na 2009 kwa usanjari huo. Riwaya nyingine alizoandika ni *Msiehena wa Mbalamwezi*, *Harufa ya Mapera*, *Tikitimaji* na *Mwandishi*, *Msomaji* na *Mchapishaji*.



Vide-Muwa Publishers

[www.vide-muwapublishers.com](http://www.vide-muwapublishers.com)

*ala eye for quality*



ISBN 9966-773-96-7

9 789966 773968

Prof Kyallo Wamitila is a renowned Kiswahili writer, who writes academic works, and fiction.